# ILE SABATO NDIO ROHO MTAKATIFU

*Waebrania 4:8-11 Maana kama Joshua angaliwapa raha, asiingelinena siku nyingine baadaye. Basi imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raho yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi yake. Basi natufanye bidii kuingia katika raha ile ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano huo wa kuasi.*

Ndugu Branham alisema: Njia pekee ambayo naitumia kufundisha Agano jipya ni kwa kutumia kivuli Agano la kale, kama vile Roho Mtakatifu hapa, anasimama kwa siku ya sabato nakadhalika. Kila kitu nyuma pale ni kivuli (waibrania 10:1) [1]

Mtu fulani aliniandikia mimi barua ambayo………. Nimeipata leo hii, na aliniuliza "Ndugu Branham, je unaishika siku ya sabato?. Nilikusikia wewe ukisema kuwa una…….asubuhi ya leo pale katika kifungua kinywa ulikula "Sauseji" na mayai nikasema, mtu mtakatifu kama wewe anakula "Sauseji"?.

Vema, ndugu, nakupenda wewe kwa moyo yangu wote, lakini kama kamwe sitatenda zaidi ya kula "Sauseji" kamwe haitanizuia kwenda mbinguni".

Angalia, ndugu, kushika siku ya sabato ilikuwa……… ni vema kama unataka kufanya hivyo. Ninaifanya kuwa kanuni mimbaranini, sizungumzii dini (dhehebu) ya mtu yeyote. Hilo ni sawa. Lakini kwa ajili ya hilo sasa ninasema hivi kule kushika siku ya sabato ilikuwa ni kivuli tuu cha ile sabato halisi. Mungu angeweza kuwapa wale sabato pale pale walipovuka Yordani. Yordani inawakilisha kifo. Na unapokuwa uko tayari kufa kabisa wewe mwenyewe, Mungu anakupa Sabato. Amina.

Nilisema "Sabato ni Roho Mtakatifu" akasema upuuzi, ile sabato ni siku. "Nikasema" Ilikuwa hivyo wakati mmoja ikiwa imewekwa kwa ajili ya watu fulani tu. Lakini leo ile Sabato ni ubatizo wa Roho Mtakatifu". Hivyo ni sawa.

Akasema, "oh, haiwezekani iwe hivyo" kwa nini? Akasema Mungu alitupatia siku na kuitia muhuri. Na kumbukumbu ya kuwa si kushika siku. Nikasema, "kwa ajili ya kundi la watu, lakini leo Waefeso 4:30 ilisema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa huyo mlitiwa muhuri mpaka siku ya ukombozi". [2]

Angalia, ndugu zetu wa Adventist (wasabato) wanasema kuwa Muhuri ya Mungu ni kushika siku ya sabato (wagalatia 4:10-11), lakini nataka mstari tu wa maandiko juu ya hilo unao onyesha ya kuwa sabato………au kushika sabato ndio Mhuri wa Mungu. Unaona, ni mtu fulani tu alitoa hilo wazo. Lakini soma Waefeso 4:30.

Umetiwa muhuri sio mpaka uamsho mwingine. Wakati umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu, hiyo ni kazi iliyokwisha kwamba Mungu amekukubali wewe, na hakuna njia ya kwenda mbali na hilo. Unasema, "Vema, nilikuwa naye na nikaenda mbali. Hapana, hukumpokea huyo. Mungu alisema inaendelea mpaka siku ya ukombozi. [3]

Ile Sabato, kama tunavyojua katika Agano Jipya, siyo kushika siku fulani. Hatuna amri / Agizo liwalo lote la kushika Jumaamosi kama sabato au kuwa na agizo la kushika siku ya kwanza ya juma ambayo ni (Jumapili), ukweli wa sabato ni huu, ambayo inamaanisha "Pumziko".

Waebrania 4:8, "Maana kama Yoshua angaliwapa raha asingaliinena siku nyingine baadaye. Basi, imesalia raha (kushika sabato) kwa watu wa Mungu kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake".

Je umesikia kile kifungu muhimu cha sehemu ya mwisho? "Mungu alivyostarehe katika kazi zake Mwenyewe".

Mungu aliwapa Israeli siku ya saba kwa ajili ya sabato yao, kwa ajili ya kumbukumbu ya kazi zake ambapo aliiumba dunia na vitu vyote vilivyomo ndani yake, na halafu aliacha

kuumba. Alistarehe katka kazi zake (Mwanzo 2:1 – 3). Alipumzika, sasa ilikuwa ni sawa kuwapa sabato ya pumziko watu waliokuwa wote mahali pamoja katika wakati, kwamba wangeweza wote kushika siku fulani. Leo nusu ya dunia jua lawaka, na nusu nyingine iko gizani, kwa hiyo haingewezekana hata kidogo. Lakini hilo ni wazo la kulinganisha katika mazingira ya kawaida.

Hebu tuone vile Biblia inatufundisha sisi juu ya hili pumziko la sabato "kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake". Huku ni kuingia ndani siyo tu kuingia ndani, lakini ni kubakia ndani ya lile pumziko. Ni "pumziko la milele" ambapo ile siku ya saba ni mfano tu.

Saba ni mwisho. Nane ni siku ya kwanza tena. Kufufuka kwa Yesu ilikuwa ni siku ya kwanza ya Juma, ikitupa sisi uzima wa milele na pumziko la milele la sabato. Hivyo tunaona sabato iliyomfanya Mungu asitupe sisi siku yoyote katka juma kama sabato (au pumziko). Tumeingia ndani na kubakia katika pumziko ambalo Israeli wasingeweza, wao walikuwa na kivuli tu cha mambo halisi ambayo tunayafuatilia. Kwa nini tuende kwenye kivuli mambo halisi tunayo sasa?

Tunaipokeaje hii sabato / au pumziko, au tunadumu na kuendelea vipi na sabato, ni katika mwaliko wa Yesu alisema.

Matayo 11:28-29. "Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo nami nitawapumzisha, Jitieni nira yangu na mjifunze kwangu……….nanyi mtapata raha ( au kushika sabato, siyo siku lakini ni uzima wa milele) nafsini mwenu".

Haijalishi mmesumbuka na mizigo mingapi ya dhambi, kama miaka kumi, miaka thelathini au miaka hamsini au zaidi, njooni na maisha yako yaliyochosha na wewe utapata pumziko lake (Sabato ya kweli). Yesu atakupa wewe pumziko.

Sasa ni nini hasa pumziko hilo ambalo Yesu atakupa? Isaya 28:8-12. Maana meza zote zimejaa matapiko na uchafu, hapana mahali palipo safi. Atamfundisha nani maarifa? Atamfahamisha nani (mafundisho) habari hii? Je ni wale walioachishwa maziwa waliondolewa matitini? Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo. La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa, ambao aliwaambia hii ndiyo raha yenu (sabato) mpeni raha yeye aliyechoka (au kuishika sabato yake) na huku ndiko kuburudika lakini hawakutaka kusikia".

Hii hapa imetabiriwa hapa katika Isaya. Na ilikuja kutimia miaka 700 baadae siku ya pentekoste wakati watu walipojazwa na Roho Mtakatifu kama ilivyosemekana kwamba itakuwa (Matendo 2:1-4). Hii ndiyo sabato ya kweli ambayo iliahidiwa kwa hiyo walipojazwa na Roho Mtakatifu walikoma waliacha kuendelea na kazi zao za dunia, matendo yao ya kidunia, Njia zao ovu.

Roho Mtakatifu akachukuwa nafasi katika maisha yao. Waliingia katika pumziko, hilo hapa pumziko lako. Hiyo ndiyo sabato yako. Siyo siku, wala mwaka, lakini ni milele iliyobarikiwa ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Ni wewe unakoma, na Mungu anafanya. Ni Mungu ndani yako kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa ajili ya kusudi lake jema. [4]

Isaya alisema kuwa pumziko lilikuwa midomo ya watu wageni na lugha nyingine atazungumza na watu hawa (Isaya 28:11). Na huku ndiko kushika sabato. Sasa unasemaje kuhusu hilo? Likoje? Lilibadilishwa wapi? Au chochote kile? Yesu alithibitisha maneno hayo hayo. Paulo katika Waebrania sura ya 4:6-11 alithibitisha jambo hilo hilo.

Hiyo ni sawa. Kule kuingia ndani kwa Roho Mtakatifu………… alisema "Maana sisi tulio na Roho Mtakatifu, "tuna…….. tulipo mpokea Kristo mioyoni mwetu, tumeacha / tumepumzikia kazi zetu, kama Mungu alivyofanya na kupumzika siku ya saba". Hiyo ni kweli. Tupo hapo, hivyo ndiyo hasa hushika sabato halisi. Unaona ninavyo maanisha. Ni pale Roho Mtakatifu anapokuja ndani, Mungu anakupa muhuri ya Imani yako (Rumi 4:10-12)

Pumziko ni nini? Ni lini lilikuja hilo pumziko? Wakati watu waliponena kwa lugha ngeni na midomo ya watu wageni (Midomo ya kugugumiza). Midomo ya kugugumiza hawakuzungumza chochote, waligugumiza. Lilitokea lini hilo? Siku ya Pentekoste wakati

Roho Mtakatifu alipokuja (Matendo 2:1-4). Hilo lilikuwa pumziko. Roho Mtakatifu Yesu alisema, "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na kuelemewa na mizigo, na mimi nitawapa pumziko. Nitawapa uzima wa milele(zoe uhai wa Mungu mwenyewe)" Mungu atakuja ndani yenu na awe sehemu yenu. Atawapa kule kuzaliwa (Yohana 3:3-8) na kukufanya mwana na binti (Wagalatia 4:6-7) [6]

Hili ndilo pumziko. Siyo jumaapili hiyo siyo siku ya pumziko. Roho Mtakatifu ndiyo siku ya pumziko. Ninyi ndugu wa Adventist (wasabato) siyo siku ya saba, sabato ni pumziko. Roho Mtakatifu ndio Pumziko. "Sabato" maana yake "pumziko". Hili ni pumziko la nafsi, una pumziko la milele. [7]

Sasa, Angalia, hilo lilikuwa pumziko la tatu analitoa. La kwanza: Mungu alilipokea kutoka kazi zake zote. La pili: Israeli walilipokea katika sheria. La tatu Kanisa lilipokea kama sehemu ya Mungu.

Nambari tatu ni namba ya uhai. Ni wangapi wanajua hilo? Kila mara ukiona nambari tatu ni uhai. Ona hili, Mungu alipoumba dunia, siku ya tatu ilikuwa ni uhai. Ni wangapi wanajua hilo? Siku ya tatu, kulikuja uhai katika siku ya tatu ya uumbaji……….(Mwanzo 1:9-13) Lile pumziko la Mungu, lile pumziko la Israeli na lile pumziko la Kanisa, kushika ile Sabato.

Kwa hiyo kamwe kama hujapokea Roho Mtakatifu bado, Bado hujaingia katika pumziko la Mungu kamwe. Huhitaji kusema, "oh, mimi siwezi, nataka kuvuta, mimi siwezi kufanya jambo hilo, mimi ni mkristo. Mimi hakika sipendi ulevi, lakini mimi ni mkristo, mimi siwezi………. Sipendi ulevi lakini bado napenda".

Kama una tamaa za wanawake, kama unafanya mambo haya yote yasiyo ya kimungu, hujafikia ule muda wa pumziko bado kamwe hujaingia katika lile pumziko lako.

Na unapoingia katika lile pumziko, unakoma au unaacha kufanya kazi zako mwenyewe za kidunia kama Mungu alivyofanya kazi zake. Kwanini? Wewe ni sehemu ya Mungu. Unapumzika milele, liko hapa, hiyo ndiyo sabato, "njooni kwangu mimi, ninyi msumbukao" [6]

Angalia hapa katika Waebrania 7:7-11, je yeye hakuzungumzia pumziko linguine? Mungu ameumba siku ya saba naye aliwapa kupumzik katika siku ya saba. Mahali pengine alizungumza juu ya pumziko alisema: leo katika Daudi…………hapo aliwapa siku nyingine ya pumziko njooni kwangu mimi, ninyi nyote msumbukao na kuelemewa na mizingo, nami nitawapa pumziko. Ingia katika hili pumziko. Maana sisi tulioingia katika pumziko hili tumeacha kufanya kazi zetu kama Mungu alivyofanya siku ya sabato. Hakika hiyo hapo sabato yako, pumziko. Hilo hapo pumziko lako halisi katika nchi hii ya ahadi. [8]

**Nukuuzakiingereza**


1. MaswalinamajibukuhusuMwanzo COD uk 51
2. Matokeoyauamuzi (55 – 1008)Aya E – 37-38
3. UleMuhuriwasabakitabu cha mihuriuk545
4. One la Patimokitabu cha NyakatisabazaKanisauk 45 -46
5. Yule mkichaawa Gadara (54 – 0720A) Aya E – 67 – 68
6. Waibraniasuraya4 (57 – 0901 E)Aya 186 – 191.
7. UhalisiwaMunguusioshindwa (60 – 06261) Aya 220.
8. KudhihirishwakwawanawaMungu (60–0518) Aya 129


---


Jiwe la kujengea la kiroho nambari 196 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendestr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.


---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:


*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*